



TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

**MASWALI NA MAJIBU KUHUSU SHERIA YA
HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KWENYE
USIMAMIZI WA SACCOS NCHINI**



“Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi”

**(I) JE, SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
IMETUNGWA LINI NA KWA LENGU GANI?**

Serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya mwaka 2018 mwezi Novemba 2018 ili kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha na kuhamasisha ukuaji na uendelezaji wa Sekta hiyo.

**(II) JE, NI LINI SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA
FEDHA ILIANZA KUFANYA KAZI RASMI?**

Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha zilitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuanza kazi rasmi mnamo tarehe 01 Novemba 2019

**(III) JE, NI LINI KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA
FEDHA ZILITANGAZWA KWENYE GAZETI LA
SERIKALI?**

Kanuni zilitangazwa kwenye gazeti la Serikali mnamo tarehe 13 Septemba 2019 GN. Na.675

(IV) JE, MTAJI WA SACCOS ZENYE LESENI DARAJA A NA B UNAANZIA KIASI GANI?

Kiwango cha chini cha mtaji kwa SACCOS zenye leseni daraja A ni Tsh Milioni 10 na leseni daraja B ni Tsh Milioni 200.

(V) JE MTAJI WA SACCOS UNAJUMUISHA VITU GANI? NA KWANINI AKIBA NA AMANA ZA WANACHAMA HAZIHUSIKI KWENYE MTAJI?

Mtaji wa SACCOS unajumuisha hisa za wanachama, matengo ya kisheria, limbikizo la ziada, faida ya mwaka husika, misaada na ruzuku isiyo na masharti ya kurejeshwa. Akiba na Amana hazihusiki kwenye mtaji kwa kuwa ni sehemu ya madeni chamani yanayodaiwa na wanachama kwenye chama.

(VI) JE, KWANI SACCOS ZOTE ZINAPASWA KUPEWA LESENI KWA MUJIBU WA SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA?

SACCOS kama taasisi nyingine za fedha zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha zinapaswa kusimamiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria hiyo kwa lengo la kupunguza changamoto za utoaji wa huduma za fedha pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa SACCOS nchini.

(VII) JE, NI SHUGHULI GANI ZINAZORUHUSIWA KUTOLEWA NA SACCOS YENYE LESENI DARAJA A KWA MUJIBU WA SHERIA?

- ◇ **Kupokea hisa za uanachama na za hiari**
- ◇ **Kupokea akiba na kutoa mikopo kwa wanachama wake.**
- ◇ **Kufanya uwekezaji**
- ◇ **Kufanya shughuli nyingine zitakazoidhinishwa na Benki Kuu au Tume ya Maendeleo ya Ushirika.**

(VIII) JE, NI SHUGHULI GANI ZINARUHUSIWA KUTOLEWA NA SACCOS YENYE LESENI DARAJA B KWA MUJIBU WA SHERIA?

- ◇ **Shughuli zote zilizoruhusiwa kwa SACCOS zenye leseni daraja A;**
- ◇ **Kupokea amana kutoka kwa wanachama wake**
- ◇ **Kutoa mikopo shirikishi**
- ◇ **Kutoa mikopo ya karadha**
- ◇ **Huduma za uwakala wa bima ndogo**
- ◇ **Uwakala wa benki,**
- ◇ **Uwekezaji wa mitaji,**
- ◇ **Kutoa kadi za malipo (debit card),**
- ◇ **Kufungua maatawi na milango ya huduma na**
- ◇ **Shughuli nyingine zitakazoidhinishwa na Benki Kuu au Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kama Mamlaka Kasimishwa**

(IX) JE, SACCOS ZINAPASWA KUANZA KUOMBA LESENI ZA USIMAMIZI KIPINDI GANI?

SACCOS zote zinapaswa kuanza utaratibu wa kuomba leseni tangu mnamo tarehe 01 Novemba 2019. Aidha, kwa SACCOS ambazo zimekuwa zikifanya kazi kabla ya kuanza kwa Sheria hii zimepewa muda wa mpito wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 01 novemba 2019 hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2020 ziwe zimeomba na kupata Leseni. Kwa SACCOS zinazoanza kazi zinapaswa kuhakikisha zinaomba na kupewa leseni kabla ya kuanza kufanya biashara ya huduma Ndogo za fedha.

X) JE, IWAPO SACCOS HAITAOMBA LESENI KWA MUJIBU WA SHERIA, ITACHUKULIWA HATUA GANI?

Kwa mujibu wa Sheria, ni kosa kuendelea kutoa huduma ndogo za fedha pasipo kuwa na leseni ya usimamizi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria hii, na iwapo itabainika, SACCOS husika itachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria

XI) JE, NI NYARAKA GANI ZINATAKIWA WAKATI WA KUOMBA LESENI DARAJA A?

SACCOS inapaswa kuwasilisha nyaraka zifuatazo;

- i. Barua au fomu ya maombi**
- ii. Masharti ya chama**
- iii. Hati au cheti cha Usajili**
- iv. Sera ya Mikopo**
- v. Sera ya uwekezaji**
- vi. Maazimio ya Mkutano Mkuu kuomba leseni**
- vii. Uthibitisho kwamba SACCOS imeajiri Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu au imeingia mkataba na mkaguzi wa ndani wa hesabu**
- viii. Mfumo wa Menejimenti ya Taarifa (MIS)**
- ix. Picha, nakala za vyeti, CV za Viongozi na watendaji wakuu wa chama.**
- x. Uthibitisho wa malipo ya ada ya sh.100,000 kwa ajili ya maombi ya leseni daraja A**

XII) JE, NI NYARAKA GANI ZINATAKIWA WAKATI WA KUOMBA LESENI DARAJA B?

SACCOS inapaswa kuwasilisha nyaraka zifuatazo;

- i. Nyaraka zote zinazotakiwa kwa ajili ya kuomba leseni daraja A.**
- ii. Mpango wa Biashara wa miaka (3)**
- iii. Sera za Rasilimali Watu, Akiba, Ukwasi, Fedha na Ukusanyaji Madeni.**
- iv. Miongozo ya Udhhibiti wa Ndani**
- v. Ushahidi wa uwepo wa bima**
- vi. Uthibitisho wa malipo ya ada ya sh.300,000 kwa ajili ya maombi ya leseni daraja A**

XIII) JE, LESENI ITAKUWA INAOMBWA NA KUTOLEWA KILA MWAKA? NA JE, ITAKUWA IKILIPWA ADA YA LESENI KWA KILA MWAKA PIA?

Leseni itatolewa mara moja tu na itadumu muda wote ambao SACCOS itakuwa inatoa huduma zake kwa wanachama kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Leseni hiyo haitalipiwa ada yoyote ya mwaka husika.

(XIV) NI SHUGHULI GANI HAZIRUHUSIWI KUTOLEWA NA SACCOS NCHINI?

- **Kuendesha akaunti ya hundi kwa wanachama,**
- **Kupokea amana kwa wasio wanachama,**
- **Kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni**
- **Shughuli za biashara za nje,**
- **Shughuli za udhamini,**
- **Kutoa credit cards,**
- **Kuhamisha fedha na kutoa oda za malipo**
- **Shughuli nyingine itakayoainishwa na Benki Kuu au mamlaka kasimishwa.**

(XV) Maombi ya leseni ya SACCOS yatawasilishwaje?

- Leseni zote zitatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini Makao Makuu ya Tume.**
- Maombi yote ya leseni yataombwa kwa njia ya mtandao (SACCOS License online Application System)**

Kwa maelezo zaidi:

Mrajis wa Vyama vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC),
S.L.P 201,
DODOMA



Tume ya maendeleo ya Ushirika



Ushirika_tcdc



@ushirika_tcdc